**LEARNING BY EAR**

**“Mihadarati na vileo – Poromoko la jamii ”**

**Episode 2: “Kijaluba cha pandora”**

**Author: Chrispin Mwakideu**

**Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**Proof reader: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: NIGHT AT CHUNGA SANA BUS STATION**

- **Jabali (m, 18)**
- **Zula (m, 18)**
- **Okosho (m, 18)**

**SCENE TWO: PUYANGA AND BERI AT HOME**

- **Puyanga (mume, 50)**
- **Beri (mke, 45)**

**SCENE THREE: OUTSIDE CLUB 2000**

- **Jabali (m, 18)**
- **Zula (m, 18)**
- **Okosho (m, 18)**
- **Chambo (m, 30)**

**SCENE FOUR: BERI ALONE AT HER HOUSE**

- **Beri (f, 45)**

**Narrator (m/f)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu katika kipindi chetu cha Noa bongo, jenga maisha yako. Hiki ni kipindi chetu cha pili katika makala kuhusiana na mihadarati na vileo vyengine kwa jina **"Poromoko la jamii".** Katika kipindi kilichopita, Jabali alifurahi baada ya kupita mtihani wake na akawa na hamu kujiunga na chuo kikuu. Pia alipawa mwaliko kutoka kwa masahiba zake waliosoma pamoja, Okosho na Zula, ili usiku waende kilabu 2000. Bamju, jambazi sugu, alitiwa mbaroni baada ya kupatikana na bangi, la kushangaza ni kuwa aliachiliwa huru masaa machache baadae, jambo lililomkasirisha Inspekta Tino. Sasa, hadithi itatuabirisha ngama ipi? Basi jumuika nasi nasi katika kipindi hiki cha pili kijulikanacho kama, **"Kijaluba cha Pandora".** Hadithi yetu inaanza saa tatu usiku katika kituo cha basi cha Chunga Sana, ambako Okosho, Zula na Jabali wanakutana kabla ya kuelekea kilabu 2000.

**SCENE ONE: NIGHT AT CHUNGA SANA BUS STATION**

1. **SFX:** **OCCASIONAL CARS DRIVING BY. HOOTING, YELLING ETC.**

2. **ZULA:** (Singing song by Black Eyed Peas- ‘I Got A Feeling’)

3. **OKOSHO:** Zula, Unanikoroga bwana. Dakika moja umjameika unaimba nyimbo za reggeae, dakika nyengine unaimba hip-hop. Ulipata majamboz yote nilokutuma ya usiku?

4. **ZULA:** Mdogo mdogo.. mamen… Zula boy akiwepo kila kitu shwari….

5. **JABALI:** Okosho, hujanieleza tutaingia vipi kilabuni. Unajuwa vyema kuwa hatujapata vitambulisho bado. Itakuaje wakituuliza vitambulisho?

6. **OKOSHO:** Jabali, hayo wewe niachie mimi. Usijali, kama Zula alivyosema, mambo yote ni bam bam.

7. **(They all laugh)**

8. **SFX: PUBLIC VEHICLE ARRIVES AND HONKS**

9. **OKOSHO:** Hili basi poa kabisa – litatushusha nje ya kilabu 2000. tupandeni. Mambo Hoyeee!

10. **SFX: PUBLIC VEHICLE DRIVES OFF/ DRIVER STEPS ON GAS**

11. **NARRATOR:** Huku maswahiba watatu wakipanda basi kuelekea kilabu, Beri, mkuu wa polisi, yuko nyumbani na mumewe, Puyanga. Puyanga alikuwa mfanyi biashara wa kawaida tu mpaka hivi punde tu, ghafla, amekuwa mkwasi ajabu. Alimwambia mkewake kuwa amejihusisha na biashara ya bandarini, na faida yake imekuwa marudufu. Lakini, je ni kweli? Hebu tuwasikilize

**SCENE TWO: PUYANGA AND BERI AT HOME**

12. **SFX: FIZZY DRINK BEING POURED INTO A GLASS(studio)**

13. **PUYANGA:** Tosha! Hiyo soda tosha, Beri! Nilitaka kidogo tu unichanganyie na kinywaji changu.

14. **BERI:** Puyanga, mumewangu. Ninajali afya yako ndio maana…

15. **PUYANGA:** **(cuts her short)** Upuuzi! Jali afya yako, afya yangu niachie mwenyewe. Kufa ni wajibu eti!

16. **SFX: PUYANGA DRINKS (studio)**

17. **BERI:** Puyanga… Umebadilika mno. Hii kazi ya bandarini ndiyo imekufunza kunywa pombe, isitoshe hivi karibuni naona unazidi kuwa chakari... na kuhofia – na sio kwa kuwa mimi ni askari polisi bali kama mkeo.

18. **PUYANGA:** **(hidden rage)** Twaweza kubadilisha gumzo?

19. **BERI:** **(UPOLE)** Mume wangu, nahofia umeanza kuwa mlevi. unahitaji…

20. **SFX: GLASS HITTING FLOOR/WALL AND BREAKING**

21. **PUYANGA:** Usiniambie ninachohitaji, mwanamke! Mimi si kurutu kituoni kwako. Ah – acha niende pahala pengine nikanywe kwa amani.

22. **BERI:** **(lovingly)** Nisamehe, Puyanga. unakwendapi? Ni usiku mwingi...

23. **PUYANGA:** **(sarcastic)** Oh, kwa hivyo masaa pia ni ya kupimiwa? Basi nitie pingu ukanifunge! **(Pause)** Kwaheri.

24. **SFX: DOOR OPENED AND BANGED**

25. **BERI:** **(between sobs)** Puyanga, hebu ngoja! Nisamehe… tafadhali ! **(more sobs)**

26. **MSIMULIZI:** Ulevi umekuwa chimbuko la maafa mengi barani Afrika- familia nyingi zimevunjika, wazazi wamesahau majukumu yao kwa watoto, watu wamepoteza ajira, matatizo ya kiafya, na hata vifo. Je, Puyanga anaelekea njia hiyo? Beri atastahimili tabia hii kwa muda gani? Je, kuna njia yeyote ya kumsaidia Puyanga na wengine kama yeye? Maswali haya yanaulizwa na familia nyingi. Lakini kabla hatujajibu, hebu tukutane na barobaro huyu anayeitwa Chambo. Yeye ni manusura wa mihadarati na vileo baada ya kupelekwa kituo cha kurekebisha tabia, na hivi sasa huwaelimisha watu kuhusu athari za mihadarati na vileo vyengine. Leo, yuko mahala muafaka – au tuseme mahala makosa… kilabu 2000.

**SCENE THREE: OUTSIDE CLUB 2000**

27. **SFX: LOCAL HIT SONG PLAYING IN BACKGROUND**

28. **ZULA:** **(excited)** Loooolo! Mamma mia…Hebu watazame wale warembo walivyoneemeka!

29. **JABALI:** Ala, Zula kumbe ukiona warembo, lahaja yako ya kijamaika huenda likizo.

30. **OKOSHO:** Hebu ningojeeni, narudi sasa hivi. Zula – usitizame warembo namna hiyo macho yatadondoka!!!.

31. **ZULA:** Aah mameni! Sitazamagi warembo, wao ndio wananitazamaga mimi, wote wamekufa kwa Zula. **(whispering)** Jabali, leo nina kitu kizito. Kwanza lakini tuanze na hiki.

32. **SFX: PAPER BEING UNWRAPPED (studio)**

33. **JABALI:** Miraa!

34. **ZULA:** Hapana, miraa *freshi*! Ukitafuna hii hutosinzia. Huu ni usiku wetu, mameni.

35. **JABALI:** **(hesitant)** Ah… Zula, nilidhani tumekuja kucheza densi na kujifurahisha.

36. **ZULA:** Furaha ndio hii! Na hiki ni kionjo tu... shika, chukua dharba. Huna haja ya kuchonga kilo nzima...

37. **JABALI:** Hapana.…siwezi… sijawahi kutafuna miraa.

38. **ZULA:** Jifunze kutoka kwangu basi... kuchanua gomba ni rahisi kama kuanguka mtihani.

39. **MSIMULIZI:** Huku Jabali akiwa nje ya kilabu anapata mafunzo ya haraka ya jinsi ya kutafuna miraa, Okosho alibidiika kutafuta njia ya kuingia kilabuni bila vitambulisho. Lakini kumbuka- Chambo yuko pale pia, kwa ruhusa ya kilabu hicho na idhini ya utawala wa mkoa, ili achunguze uwepo wa vijana wadogo wasiostahili kuwa pale.

40. **(MUSIC STILL PLAYING IN BACKGROUND)**

41. **OKOSHO:** **(signals to CHAMBO)** Sasa! Pssss.. leo inakuwaje? Hmm. Chukua paketi ya sigara. Leo tuko wa tatu sio wawili kama kawaida.

42. **CHAMBO:** Bahati mbaya kijana, nimeacha kuvuta sigara. Kwanini pia wewe usiache, sigara hudhuru afya yako.

43. **OKOSHO:** Sawa, kwa hivyo hutaki sigara? Sasa wataka nini? Nina miraa, pombe na… wajua nini eh? Kitu chenyewe! Bangi! nimejiseti vizuri sana. Tuache tuingie!

44. **CHAMBO:** Sikiliza. Jina langu ni Chambo. Nafanya na shirika la Youth Watch organisation, na tunajaribu kuwasaidia vijana kama nyinyi….

45. **OKOSHO:** **(cuts him short)** Hebu – ngoja nikaite rafiki zangu. **(to himself)** Hatuwezi kukosa raha zote hizi…

46. **SFX: Footsteps leaving**

47. **OKOSHO:** **( calls out to ZULA and JABALI )** Oyee, Jabali, Zula - njooni!

48. **SFX: ZULA WITH MOUTH FULL OF KHAT**

49. **ZULA:** **(in between chewing)** Mbona umekawia sana leo.

50. **JABALI:** Yaonekana nyinyi wawili si wageni hapa kabisa.

51. **ZULA:** **(still chewing)** Watuchukuliaje wewe? Hata kama hatuna vitambulisho.. sisi ni member bila vibali...

52. **OKOSHO:** **(not impressed)** Zula, Nani amekwambia ufungue huo mfuko? Nani amesema muanze bila mimi?

53. **ZULA:** Hakuna. Tuliboeka tukaona vyema tujitulize.

54. **OKOSHO:** Na mbona Jabali ameshika miraa yake kama ambayo ni sumu?

55. **ZULA:** Amejaribu jani moja, akalitema. Adaisha ni chungu. Namwambia angezidi kutafuna angelisikia ladha ikigeuka ikawa kama ya asali.

56. **JABALI:** La, haya si mambo yangu, Zula. Okosho, hatuingii ndani ama? Muda wayoyoma.

57. **OKOSHO:** Tutaingia , lakini mpango umegeuka kidogo tu. Sikilizeni.

58. **MSIMULIZI:** Okosho aliamua lazima waingie kilabu 2000. Amejihami nakila aina ya mihadarati, ambayo yeye na Zula wamekuwa wakitumia kwa muda. Sasa walitaka kumshawishi Jabali awe mtumiaji pia. Okosho alikusanya wenzake chap chap na kuwaeleza jinsi wangeingia kilabu. Kwengineko, Beri bado anahukumika na maongezi yake na Puyanga. Akajaribu kutazama runinga ili kujiliwaza lakini wapi, akaenuka na kuelekea chumba chao cha malazi…

**SCENE FOUR: BERI ALONE AT HER HOUSE**

59. **SFX: TV SET RUNNING IN BACKGROUND**

60. **BERI:** Hiki kipindi chasinya.

61. **SFX: TV SET SWITCHED OFF**

62. **BERI:** **(monologue)** Mumewangu simuelewi tena siku hizi. Au ana mpango wa kando? Ni biashara gani hizi ambazo ni msiri nazo? Lazima nichunguze, siwezi kuishi hivi… wacha nifunge mlango wa mbele - sijui atarudi saa ngapi!

63. **SFX: DOOR LOCKED SHUT**

64. **BERI:** Sawa. Wacha nione muna nini humu kwenye droo, kama ananidanganya, nina hakika ya kupata ushahidi. Mungu wangu! Je kama ana mwanamke mwengine? Nitayaweza kweli? Na hili tatizo sugu la ulevi wake? Au ni hizo kazi zake ndizo zinampa matatizo?

65. **SFX: DRAWERS BEING OPENED AND CLOSED.**

66. **BERI:** Ameifunga! Mbona hii droo ya chini imefungwa? Nilifanya vizuri kughushi funguo zote za nyumba hii.

67. **SFX: KEY OPENING DRAWER. THEN DRAWER PULLED OUT.**

68. **BERI:** **(in utter shock and disbelief)** Hapana! Haiwezekani ! Siamini la… laaaaa… **(BERI'S denials fade away amidst sobs)**

**OUTRO:**

Wa jadi walinena, shauku ilimuua paka… Beri alijihisi zaidi ya huyo paka alipofungua droo ya mumewake. Alijua bayana kuwa maisha yake, ndoa yake, au hata ajira yake ya uaskari itachukuwa mkondo mpya. Lakini ameona nini? Ataweza kumkabili mumewe, Puyanga? Katika kilabu 2000, vijana wetu watavuka wavu wa Chambo? Okosho ana mpango gani wa usiku ule ambao Jabali haufahamu? Haya na mengine ni katika kipindi kifuatacho kinachohusu ubadirifu wa mihadarati na vileo vyengine. Kusikiliza tena au kutuoa maoni tembelea tovuti yetu www.dw.de/lbe mpaka wakati mwengine, jiepushe na mihadarati.